
Michango ya kamati, bila daftari.

Ahadi ni mfumo wa kufuatilia michango ya sherehe. Kamati inaandika kila ahadi na kila malipo sehemu moja, na mfumo unatuma vikumbusho wenyewe kwa SMS na WhatsApp. Siku ya kikao, ripoti iko tayari.


> **Fedha haipiti Ahadi.**
>
> Michango inaenda moja kwa moja kwenye namba au akaunti ya kamati yenu. Ahadi ni daftari linalokumbuka na kukumbusha, siyo benki. Hatushiki fedha ya mtu hata siku moja.

Mnachohitaji


- Simu au kompyuta yenye intaneti, kwa wanakamati pekee.
- Majina na namba za simu za wachangiaji.
- Wachangiaji hawahitaji akaunti, app wala smartphone. Wanapokea SMS ya kawaida.



Dashibodi: ahadi zote, zilizolipwa, salio na waliochelewa.



Rejista: kila mchangiaji na hali yake.



Vikumbusho: ujumbe unaotumwa na uliokwishatumwa.

Hatua nane

1

Fungua akaunti

Nenda ahadi.cardstz.co.tz, bonyeza "Fungua akaunti". Weka jina lako, barua pepe na nenosiri la herufi nane au zaidi. Utapokea barua pepe ya kuthibitisha. Akaunti ni kwa wanakamati pekee.

2

Tengeneza tukio

Bonyeza "+ Tukio". Weka jina la tukio, tarehe yake na lengo la fedha mnalolikusudia.

3

Weka njia za kulipia

M-Pesa, Mixx, Airtel Money, Halopesa au akaunti ya benki. Mnaweza kuweka hadi nne. Hizi ndizo zinazoonekana kwenye kila ujumbe unaomwendea mchangiaji.

4

Andikisha wachangiaji

Nenda Rejista. Weka jina, namba ya simu, kiasi cha ahadi na tarehe ya kulipa. Mchangiaji anapokea ujumbe wa uthibitisho papo hapo, wenye namba za kulipia.

5

Mna orodha tayari?

Si lazima muandike upya. Pakia faili la Excel au CSV, au piga picha ya daftari lenu la mkono. Ahadi inaisoma na kuipanga yenyewe, kisha mnahakiki kabla ya kuhifadhi.

6

Andika malipo

Nenda Malipo, chagua mtu, andika kiasi alicholipa na njia aliyotumia. Risiti yenye salio lililobaki inamwendea yeye mwenyewe mara moja.

7

Vikumbusho vinajituma

Mfumo unaangalia kila siku asubuhi na kutuma kwa wanaostahili: siku tatu kabla ya tarehe, siku yenyewe, kisha kila wiki hadi alipe. Hamhitaji kumpigia mtu simu.

8

Shiriki na kundi, kisha ripoti

"Shiriki na kundi" inatoa link ya kusoma tu ya kubandika kwenye kundi la WhatsApp. Inajisasisha yenyewe na haionyeshi namba za simu. Siku ya kikao, Ripoti inakupa PDF au Excel.

Maswali yanayoulizwa

Je fedha inapita kwenu?

Hapana, na haitapita. Michango inaenda moja kwa moja kwenye namba au akaunti mliyoweka.

Mchangiaji hana smartphone?

Anapokea SMS ya kawaida. Hahitaji app, intaneti wala WhatsApp.

Nani anaona orodha?

Wanakamati wenye akaunti, na yeyote mwenye link ya kusoma tu mliyoituma kundini. Mkitaka, mnatengeneza link mpya na ya zamani inakufa.

Namba moja inaweza kubeba ahadi zaidi ya moja?

Ndiyo. Mfano baba akiwawekea watoto wake wote kupitia namba yake.

Mtu akitaka asikumbushwe tena?

Anajibu neno ACHA kwa WhatsApp, na vikumbusho vyake vinasimama papo hapo.

Mchangiaji anaweza kujua salio lake?

Ndiyo. Anaandika SALIO kwa WhatsApp na anapata jibu mara moja.

Taarifa zinakaa muda gani?

Miezi kumi na miwili baada ya tukio kufungwa, kisha zinafutwa. Sera kamili ipo ahadi.cardstz.co.tz/sera.

Gharama ni kiasi gani?

Tupigie, tuzungumze kulingana na ukubwa wa tukio lenu.

Mnataka kujaribu?

Tupigie WhatsApp, tutawafungulia tukio lenu la kwanza na kuwaonyesha hatua kwa hatua.

WhatsApp 0689 786 819 **ahadi.cardstz.co.tz**